






## Utawala Bora wa Misitu

Rasilimali za misitu zinasaidia kuendesha maisha ya watanzania wengi. Kwa sasa uvunaji uliozidi kiwango, matumizi mabaya, na utawala dhaifu umekwaza uwezo wake wa kuchangia lengo kuu la maendeleo la taifa. Taarifa ya mwaka 2007, iliondaliwa na TRAFFIC, imeonyesha dhahiri mapungufu makuwa ya kijamii, kimazingira na kiuchumi katika biashara ya magogo Tanzania. .

Kampeni ya Mama Misitu, kupitia washirika wake, wameainisha vyanzo vya mapungufu katika utawala bora wa misitu ambayo kampeni hii inakusudia kuyaweka wazi:

- Wanajamii hawana ufahamu wa kutosha kuhusiana na haki zao katika misitu na ardhi ya misitu;
- Sera na Sheria za misitu na hazitekelezwi ipasavyo;
- Utawala wa sheria ya ardhi haufahamiki ;
- Usimamizi huria katika wa sekta ya biashara ya mazao ya msitu.
- Kuwapo kwa udanganyifu na vitendo haramu katika mlolongo mzima wa biashara ya magogo,

## Mama Misitu | Historia fupi

Kampeni ya Mama Misitu ilizunduliwa kwa mara ya kwanza 2008 na Kikundi Kazi cha Misitu Tanzania-TFWG, ambapo uliongozwa na Jumuiko la Maliasili Tanzania-TNRF. Mnamo mwezi Julai 2012, Kampeni ya Mama Misitu ilizunduliwa tena rasmi kwa kipindi cha miaka 5 ikiwa ni kuendeleza uelewa na kupanua wigo wa kampeni kutokana na uzoefu na yaliyojiri katika kipindi cha majaribio cha mradi.

## Mama Misitu | Lengo kuu

Kuleta mageuzi chanya ya utawala bora katika misitu and kupunguza uvunaji haramu wa misitu pamoja na kuongeza faida zitokanazo na misitu kwa jamii ziishizo kando ya misitu..

## Mama Misitu | Dhumuni

Kampeni ya Mama Misitu inalenga kuboresha utawala bora katika misitu, ili watanzania wafaidike zaidi kutokana na usimamizi endelevu wa misitu.

## Mama Misitu | Washirika wenza

Washirika wenza wanaotekeleza kampeni ya Mama Misitu ni 11 ambao wataipeleka katika ngazi ya Wilaya na Taifa. Wanaoendesha kwa ngazi ya Taifa ni LEAT, TNRF, Femina HIP, MJUMITA, JET, Policy Forum na TRAFFIC na kwa Wilaya ni TFCG, MCDI, WWF na WCST. Katika kila Wilaya kampeni itafanya uhamasishaji na kujenga uwezo katika kuboresha utawala bora wa misitu.

## Mama Misitu | Maeneo ya Utendaji

Miaka mipya 5 ya Kampeni ya Mama Misitu itafanya kazi katika wilaya 4; Rufiji, Kilwa , Kisarawe na Kibaha kabla kufikia kwenye idadi ya Wilaya 8.

Kwa upande wa Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini, kampeni itafanya kazi na vijiji vya Bokomnemela, Soga na Kipangege kwa Wilaya ya Kibaha na vijiji vya Kifuru, Mtamba, Chakenge na Kibwemwenda pamoja na vitongoji viwili vya Kola (kijiji Kisanga) na Malangalanga (kijiji Mzenga B) vya wilaya ya Kisarawe

## Mama Misitu | Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini

TFCG itatekeleza Kampeni ya Mama Misitu kuzunguka msitu wa hifadhi Ruvu Kusini kwa Wilaya za Kibaha na Kisarawe.

Mradi una malengo yafuatayo kwa Ruvu Kusini:

- Jamii waishio kando ya msitu wa ruvu kusini wana ufahamu juu ya masuala ya utawala bora wa misitu na thamani ya mazao ya misitu; Kujenga ushawishi wa kujua haki zao na wanahusishwa katika kupambana vitendo vya uharifu wa misitu.
- Kiwango cha utawala ubora katika misitu kwa Halmashauri za wilaya na vyombo vya usimamiaji wa sheria kinaimarika na kuongeza ufanisi


Mradi ungependa kuona:

- Halmashauri za wilaya zinapunguza matukio ya uhalifu wa misitu na kutimiza majukumu na wajibu wao na kukamilisha mchakato wa usimamizi wa pamoja wa misitu;
- Wakala wa huduma za misitu Tanzania na halmashauri za wilaya wanaitika wito kwa haraka juu ya taarifa za matukio ya uharibifu wa misitu.
- Kuongeza matukio ya mashitaka na hukumu za uharifu wa misitu.
- Wanaume na wanawake vijijini wanashiriki katika uhifadhi wa misitu ya vijiji kwa njia ya usimamizi wa pamoja wa misitu.
- Jamii inajiamaini kupitia utawala bora wa misitu, kutetea haki zao na kuhoji taratibu za sheria juu ya rasilimali za misitu zinazotoka katika maeneo yao.
- Jamii wanatatua matukio ya uharibifu wa misitu katika ngazi ya kijiji na kutoa taarifa kwa Wakala

wa Huduma za Misitu Tanzania au halmashauri za wilaya.

- Jamii inatekeleza wajibu na majukumu yao kupitia usimamizi wa pamoja wa misitu.

## Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini | Uharibifu



*Ramani inayoonyesha uharibifu wa misitu Ruvu Kusini*

Kati ya miaka 2000 na 2011, karibia 40% ya Misitu ya ukanda Pwani Ruvu Kusini imepotea (Sehemu nyekundu katika ramani). Uharibifu mkubwa umetokea kusini magharibi jirani na shamba la Jetropha. Uvunaji haramu wa mkaa na magogo ndio chanzo kikubwa cha uharibifu huo. Kwa viwango vya vilivyopo sasa, msitu wote wa Ruvu Kusini utakuwa, umekwisha ifikapo mwaka 2035.

## Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini | Thamani

Ruvu Kusini inaunda ukanda wa kijani wa jiji la Dar es salaam na unajukumu muhimu la kurekebisha ubora wa hali ya hewa; upatikanaji na usambazaji wa maji katika jiji. Vilevile ni sehemu ya misitu ya ukanda wa Pwani yenye wingi wa bioanuwai muhimu na ni makazi ya wanyama adimu waliohatarini kutoweka ambao wanapatikana katika misitu saba tu ya Tanzania

## Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini | Uhifadhi

Kwa kipindi cha miaka ya 2000 na 2006, TFCG ilifanya kazi na jamii, Idara ya Misitu na Nyuki (TFS) na halmashauri za wilaya kuanzisha usimamizi wa pamoja wa misitu. Mipango ya uendeshaji, sheria ndogo na mikataba ya makubaliano iliandaliwa. Nyaraka zote zilisainiwa na wanajamii, kata na halmashauri za wilaya. Hata hivyo Idara ya Mistu na Nyuki kwa sasa Wakala wa Huduma za Misitu hawakuweza kusaini nyaraka hizi hadi sasa..

## Kuhusu Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Ni shirika lisilo la Kiserikali lenye lengo la kuhifadhi na kurejesha misitu nyenye bioanuwai muhimu kitaifa na kimataifa kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho. TFCG inafanya kazi na jamii pamoja na wadau wengine waliopo kando ya milima ya Tao la Mashariki na Ukanda wa Pwani. www.tfcg.org tfcg@tfcg.or.tz
PO Box 23410, DSM

## Kuhusu SHIWAMARU

Shirikisho la Wakulima na Watetezi wa Mazingira Ruvu Kusini (SHIWAMARU) ni mtandao ambao uliundwa mwaka 2001 na kusajiliwa mwaka 2011. Dhumuni la mtandao huu ni kuvileta pamoja vijiji vinavyozunguka Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini ili kuweza kushirikiana, kutunza na kuhifadhi msitu huu. Mtandao unafanya kazi wilaya za Kibaha na Kisarawe katika vijiji vya Soga, Kipangege, Mpiji, Bokomnemela, Kibwemwenda na Kitongoji cha Malangalanga. Makao makuu ya mtandao huu yapo kijiji cha Soga, kata ya Soga S.L.P 30180.

## Kuhusu UWAMIRU

UWAMIRU
Umoja wa Watetezi wa Misitu Ruvu Kusini

Umoja wa Watetezi wa Misitu ya Ruvu Kusini. (UWAMIRU) ni mtandao ambao uliundwa mwaka 2002. Dhumuni la mtandao huu ni kuvileta pamoja vijiji vinavyozunguka Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini ili kuweza kushirikiana, kutunza na kuhifadhi msitu huu. Mtandao huu unafanya kazi katika wilya ya Kisarawe katika vijiji vya Mtamba, Kifuru na Chakenge. Makao makuu ya mtandao huu yapo kijiji cha Kifuru, kata ya Kisarawe S.L.P 30153 Wilaya ya Kisarawe Mkoa Pwani.

# Kampeni ya Mama Misitu katika Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini

**Tumerithi. Tuwarithishe.**



Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Mama Misitu
Tumerithi Tuwarithishe